




Diaspora Council of Tanzanians in America

Machi 20, 2021

**Buriani Mh. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



Taasisi ya Diaspora Council of Tanzanians in America (DICOTA) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea Machi 17, 2021 katika hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam.

Uongozi wa DICOTA, pamoja na wanachama wa DICOTA, tunatoa salamu za pole kwa wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba huu mkubwa sana kwa Taifa letu. Hakika Taifa letu limepoteza kiongozi Mzalendo na Shupavu, akiwa na umri mpevu wa miaka 61.

Tunatoa pia pole za kipekee kwa ndugu wote na pamoja na familia ya marehemu.

Kwa niaba ya DICOTA tunafikisha salamu hizi za rambirambi kwa WaTanzania wote, popote pale walipo, ndani na nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"BWANA AMETOA NA BWANA AMETWAA, JINA LAKE LIHIMIDIWE."

Dkt. Frank Minja  
Rais, DICOTA

Bi. Asha Nyang'anyi  
Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, DICOTA